



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI**  
**(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)**



**MKOA WA KILIMANJARO**

Simu : 27-29 74369

Fax : 27- 29 74368

Email ded@haidc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,  
3BR-TTCL-KANISANI  
25382. BOMANG'OMBE  
S.L.P 27  
HAI ,KILIMANJARO.

**UFAPANUZI JUU YA MATUMIZI YA FEDHA ZA MFUKO WA**  
**KUCHOCHEA MAENDELEO YA JIMBO KATIKA JIMBO LA HAI.**

Jumamosi, Novemba 05, 2022.

Kufuatia kuwepo kwa taarifa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu matumizi ya fedha za mfuko wa Jimbo wilaya ya Hai.

Kumekuwa na madai kuwa Mbunge wa Jimbo la Hai ameamua kuwa matumizi ya fedha za mfuko huo ni zake, kuna usiri katika matumizi ya fedha hizo, kutokuwepo kwa kamati inayojumuisha madiwani wote na watendaji wa taasisi za kiraia.

**Ukweli ni kwamba:** - fedha za mfuko wa Jimbo ni fedha za Serikali na utaratibu wake umeainishwa katika sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kifungu cha 10(1) inataka kuwepo kwa Kamati ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo katika kila Halmashauri na kutaja wajumbe wa kamati hiyo kuwa pamoja na;

1. Mheshimiwa Mbunge wa kuchaguliwa katika Jimbo husika ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati;
2. Afisa Mipango wa Halmashauri ndiye Katibu wa Kamati;
3. Madiwani wawili katika jimbo husika ambapo mmoja lazima awa mwanamke;
4. Watendaji wa Kata wawili ambao wanafanya kazi katika Jimbo husika;
5. Mjumbe mmoja ambaye atateuliwa kutoka katika Asasi Zisizo za Serikali (Non-Governmental Organisation katika Jimbo husika.

Hivyo kamati tajwa hapo juu kwa mujibu wa sheria ipo na inafanya kazi kama sheria ilivyo elekeza na si kweli kuwa wajumbe wa Kamati hiyo wanapaswa kuwa madiwani wote na watendaji wa taasisi za kiraia.

Kuhusu Mbunge kutumia fedha hizo kwa matumizi binafsi, ni jambo ambalo haliwezekani kwa kuwa fedha hizo huingizwa kwenye akaunti ya Halmashauri na hutolewa kwa kufuata taratibu za fedha za Umma hivyo haliwezi kuwa suala la siri na binafsi. Pia Halmashauri haijapokea malalamiko yoyote kutoka kwa madiwani juu ya mfuko huo.

Mapendekezo ya miradi inayotekelezwa na fedha za mfuko huo, hupokelewa kutoka ngazi ya Kata kupitia kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kata ambayo mwenyekiti wake ni Diwani wa Kata husika, maamuzi hufanyika na Kamati ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya jimbo na taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo huwasilishwa katika vikao vya kisheria ikiwa

ni pamoja na kikao cha kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango pamoja na kikao cha Baraza la Madiwani.

Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ilipokea fedha za Mfuko huo Tsh.43,951,000.00 na kwa kufuata taratibu zilitumika kutekeleza miradi mbali mbali katika vijiji vifuatavyo, Isawero, , Mjongweni, Mtakuja, Roo sinde, Sanya Station na Tindigani miradi katika shule za Msingi zifuatazo Elerai, Kyeri, Lambo Extended, Lemira, Masama Tema, Miaseni, Mkwarungo, Mlima Shabaha, Naluti, Narumu, Nkuu, Nkwannara, na Ulali na katika shule za sekondari zifuatazo Bomang'ombe, Kyuu, Lemira, Mailisita, Mukwasa, Neema na Nkokashu.

Miradi mingine ni Mfereji wa muro na kalali na mahakama ya mwanzo Machame Kaskazini.

Imetolewa na



Riziki G Lesuya  
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
Wilaya ya Hai